# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA MAKAMU WA RAIS

## BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

**29 Januari, 2026**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kibali cha ajira cha Katibu Mkuu (Utumishi) chenye Kumb. Na. FA.12/109/02/03, anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi zifuatazo;-

1. **NAFASI YA KAZI -** Dereva Daraja la II (Driver Grade II) - Nafasi 5

2. **MAJUKUMU YA KAZI**

   i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari;
   ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi;
   iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari;
   iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali;
   v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari;
   vi. Kufanya usafi wa gari; na
   vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

3. **SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji awe amehitimu Kidato cha nne (Form IV) na kupata Cheti cha ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha nne (IV). Awe na Leseni ya Daraja la 'E' au 'C' ya uendeshaji magari pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua Mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali, pamoja na vyeti vya mafunzo

vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika na awe amehudhuria mafunzo ya Msingi ya uendeshaji Magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

4. **NGAZI YA MSHAHARA** - PGSS 2

5. **AINA YA MKATABA WA AJIRA -** Ajira ya Mkataba wa mwaka mmoja(1).

6. **MASHARTI YA JUMLA**

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini serikalini.
2. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
3. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
4. Waombaji kazi ambao ni waajiriwa katika Utumishi wa Umma, WASIOMBE na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyopo katika waraka namba CAC45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba 2010.
5. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kuzaliwa, kidato cha Nne, kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho, na vyeti vya kuhitimu mafunzo udereva
6. "Testmonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
7. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

7\. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 13 Februari,2026.

8\. Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa

Mkurugenzi Mkuu, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC), Mikocheni - Mtaa wa Regenti - Kitalu Na. 28-30, S. L. P. 63154, Dar es Salaam,

9. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika Tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.

Dkt. Immaculate S. Semesi

**MKURUGENZI MKUU**

DIRECTOR GENERAL
NATIONAL ENVIRONMENT
MANAGEMENT COUNCIL(NEMC)
35 REGENT STREET
P.O.Box 63154, DAR-ES-SALAAM